Kwako Bibi

Siri ya mkoba

Wakati twajitembeza njiani, twapigwa na bumbuazi kuona kama kila mama awe kazini ama hapana apenda sana kubeba mkoba (sac à mains).

Zamani za kale, mkoba ulikuwa wa kubeba vitu vya lazima kama vile vya mtoto mchanga wakati mamaye amubeba kwa mganga ama aenda kutembea naye fasi ya mbali.

Kidogo kwa kidogo, mambo yakabadirika. Mkoba ukawa sasa kama vile chombo cha kuongeza urembo. Ukipita mikoani, utakuta ule binti ao mama anayeenda sokoni ama kazini haizuru wapi yupo na mkoba mkononi mwake ama mabegani.

Mkoba huo wafichika vitu vingi. Kulingana na mbinu za kisasa, kina mama wapashwa kuitimia kwa kubeba makartasi zab za lazima kwa mfano vyeti vya utambulisho (carte pour citoyen) ao vya mganga, feza na vingine.

Kama akina mama wengi hubeba ndani ya mkoba vitu vyote vya urembo (maquillage) sawa vile kio, kichanua, rangi ya midomo (rouge à lèvres), tilo na vivi hivi wengine hubeba ndani vitu visivyo kuwa na maana kamili. Ukipima kuwauliza vitu vile vyote vina mafaa gani, hujibu mbiyo eti "on n'est pas belle pour rien". Maana yake, bila kufanya nguvu, ni kugumu binti apendeze.

Wengine hubeba hata vitabu ndani ya mikoba yao kusudi ivimbe na iwe mzito. Wamoja moja hasa wale wa ndumba hubeba ndani vikwembe na wakati huwaona kwenyi vilabo, utawaona kutoka penyi giza kubadirisha mavazi sawa kinyongo ili wavute wanaume.

Ndiyo maana kina mama husema kama haifai kufungua mkoba wa mwanamke kwani unaficha siri nyingi na hata waweza kufungua macho ya wale wenyi kupenda kuona kila kitu. Tuonavyo sisi kutembea na mkoba si vibaya. Sababu yasaidia kubeba vitu vimoja vimoja visivyoweza kubebwa mkononi.

Lakini siyo kisa cha kubeba mkoba unao ukubwa wa sanduku ao wenyi beyi kali. Kwani siku hizi twaona hata wanafunzi wanaopewa na wazazi wao mikoba yenyi samani (valeur) kubwa na ambamo wanabeba mabenye na vikwembe vya kuvaa wakipotoka masomoni. Siyo kupevusha wasichana hivyo?

Bibi wa sasa akiwa na mkoba wake, ingefaa uwe mkoba wa heshima na wenyi mafaa kamili. Usiwe mkoba wa kuficha ndani dawa za mapenzi ao vitambaa vya ovyo ovyo !

Alamsiki

Bujiriri Mwangaza.

JUA

Gazeti la Kivu

Habari za popote

Kinshasa

Mipango mipya kwa kutangaza enjili

Tangu tarehe 7 hadi 14 aprili iliyopita, wachungaji (pasteurs) wa makanisa mbali mbali ya kiprotestanti walikusanyika kwenyi "Lycée Dr Shaumba" mjini Kinshasa. Mazumuni (but) ya mkusanyo huo, ilikuwa kutafuta jawabu (solution) kwa mipango mipya ya kutangaza injili nchi Zaïre. Punde tu baada ya kumalizika kwa kazi za mkutano huo, tulipokelewa katika masimulizi na mchungaji Mundyo Mwenelusiba makamu wa prezidenti wa muungano ya makanisa ya kiprotestanti jimboni (ECZ) ambaye pia ni kiongozi wa kanisa CECA. Mwananchi Mundyo alisema kuwa waprotestanti wametoka kujipatia jukumu la kuwafikia watu wote ambao bado hawajasikia habari ya Yesu Kristu. Wanataraji kufikia jukumu hilo kwa muda wa miaka mitano ijayo. Mkusanyo huo wa Kinshasa uliwahimiza na kuwafundisha namna ya kuwatafuta na kuwafikia watu wa makabila mbali mbali.

Kati ya watu ambao hawajasikia habari ya Yesu Kristu kuna wale ambao wanaotoka katika makabila madogo madogo ambayo yanazarauliwa. Wengine hubaki katika vijiji vinavyopatikana mbali kabisa na miji mikuu. Watangazaji wa injili wanaazimishwa kuwatambua na kuwaonyesha upendo wa Mungu. Ni jambo la kushangaza kuona kuwa katika miji mikuu kuna pia watu ambao hawapendi hata kidogo kusikia habari ya Yesu. Miongoni mwa watu hao twaweza kutaja kwa mfano madereva wa taxi pamoja na wanafunzi wa Univasti. Watu hao wapo hakika kwamba mambo ya dini hayaweelekei na hayana maana.

Kwenyi semina hiyo, mchungaji Mundyo alikuwa mwenyi kusindikizwa na mwananchi Kabutu Nshimbirwe katibu wa ECZ jimboni mwa Kivu. Kwa upande wake, ndugu huyo alitupasha kuwa ni dalili (preuves) za kushindwa kuona kuwa baada ya miaka zaidi ya 100 nchini humu kanisa halijulikane katika mikoa mingi. Ametaja nafasi kama vile Mayumbe, Ubangui, Bateke, ambako wetu wengi waishi kwa hali ya ushenzi.

Kanisa la ECZ litajikaza ufikapo mwaka 1990 kwa kuwatuma mwalimu mmoja wa Injili katika kila kijiji. "Kazi ni nyingi na watu wengi wahitaji kuokolewa", alimaliza kusema ndugu Kabutu.

Lubunga B. M'Kyoba.

Liban

Ingawa waaskari toka Israëli wamerejea makwao mabomu yaendelea kutwangwa, kuharibu makao, vitu, kuumiza na kuua watu kazaa.

Lakini jambo muhimu ni lile la kubadilishwa kwa wafungwa wa - Israëli wa 3 kwa wa - Jordania 1.056 mjini Geneva (Uswisi), Damas (Syria) na Gaza chini ya uchunguzi wa Msalaba Mwekundu (Croix Rouge). Mpango huo waitwa "Galilea".

Kivu ya Kaskazini

Viongozi wa "PLZ" watesa watumishi

Presidenti wa chama jimboni aliye pia Liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba alitembelea katika siku zilizopita shirika "PLZ" linalopatikana katika mtaa wa Rutshuru, jiji la Mweso. Ukomo wa safari yake huko Mweso ilikuwa ya kuwavika palata watumishi wa PLZ.

Liwali Mwando alitambua wazi kuwa watumishi wa shirika hilo la kutengeneza chai waangamizwa vikali. Watumishi hao waliamua kutuma watoto wao nafasi ya sherehe kwa kuonyesha wazi kwa liwali Mwando kuwa hawana amani na kuwa waangamizwa na wazungu wanaosimamia shirika lao.

Mwenyekiti wa jimbo la Kivu na ujumbe uliomsindikiza walijionyea wenyewe hali ya watumishi wa PLZ na kukumbuka hotuba ya Baba wa Taifa : "Huko mashariki, jimboni mwa Kivu, walimaji wa chai watembea miguu wazi wakati viongozi wa PLZ wanaouza chai hiyo katika nchi za kigeni wajiruhusu kuishi na ustarehe katika nyumba nyororo". Watumishi hao ambao walionekana kuwa wateswa na njaa kali, walifika mbele ya liwali Mwando katika hali ya kitisho, miguu kanya wakionekana wenyi kuchoka na kazi za mashamba wakingoja siku zao za mwisho kisha kufyonzwa nguvu zote na viongozi wa PLZ. Uchunguzi uliofanywa ulioleta matokeo ya kuwa mtumishi anayepokea mshahara wa kutosha anapewa kila mwisho wa mwezi zaïre 500. Watumishi wa huko waonekana wenyi sura ya kukasirika kutokana na kazi ngumu pia mshahara wa ulozi wanaopata kutoka kwa viongozi wao. Hakuna hata barabara iliyotengenezwa kwa kujielekeza kunako shirika hilo. Ujumbe wa Liwali Mwando ulifanya saa nne kwa gari kwenyi barabara inayounga PLZ na barabara kuu. Barabara hiyo ina kitambo cha kilometri 10.

Prezidenti wa chama jimboni alishikwa na hasira mpaka akakataa kuhuzuria mashamba na viwanda vya shirika hilo. Aliongeza kusema kuwa viongozi wa shirika PLZ waleta ukoloni mambo leo (néo-colonialisme) nchini Zaïre, ingawa Baba wa Taifa aliomba kwa yeyote ahusike na maendeleo ya nchi yetu. Jamaa hao wazungu hawahusike hata na kazi za kutengeneza masomo, duka hospitali na kuwafurahisha watumishi wao. Bila kusahau kutengeneza mabarabara. Liwali Mwando aliwahidia wafanya kazi kuwa mambo yote yanayotendeka huko yataweza kubadilika katika siku za usoni ndio apate kuwajia tena.

Kaboyi Habimana

Kivu ya kusini

Diosezi ya Uvira yakosa askofu

Habari zilizoletwa ofisini mwetu na kiongozi wa gazeti "JUA" huko Uvira, mwananchi Musemi Kilondo zaeleza kuwa tangu Julay 1984 diosezi ya Uvira haina askofu. Hali hiyo ilitukia kisha kujiuzulu kwa askofu Okechu kutoka Bunia na kuacha kazi kwa askofu Djehu ambaye pia aliacha diosezi yake na kurudi Bunia, jiji lake la kuzaliwa. Mbele ya kurudi Bunia askofu Djehu alimuachia madaraka padri Gapangwa. Mpaka sasa ni padri Gapangwa ndiye ahusika na uongozi wa diosezi ya Uvira akingoja wakati Baba mtakatifu wa Roma, Papa Yohana Paulo wa pili atakapomtaja askofu mwengine.

Huko Uvira watu hunongonezana kuwa Baba mtakatifu wa Roma hatashita kumtaja askofu mzaliwa wa wilaya ya Kivu ya Kusini kusudi ya kuongoza diosezi ya Uvira. Katika majina yanayotajwa na waumini wa dini ya kikatoliki muna hasa mapadri Bukanga, Gapangwa, Mutimanwa pamoja na Mugadja.

Waumini wa dini hiyo wapendelea kuona Baba mtakatifu wa Roma awatolee askofu mpya mbele au wakati wa ziara yake ya mwezi wa nane nchini Zaïre.

Kaboyi Habimana